JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

UHURU NA UMOJA

## TANGAZO LA NAFASI ZA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI NA MSINGI KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027

## 1. UTANGULIZI

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) anatangaza nafasi za Mafunzo ya Ualimu ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Msingi. Mafunzo yatakayotolewa ni Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali, Msingi na Elimu Maalumu (Miaka 02), Stashahada Maalumu ya Ualimu Elimu ya Msingi (Miaka 03) katika masomo ya Sayansi na Hisabati pamoja na Stashahada ya Elimu ya Ualimu Elimu ya Awali na Msingi kwa njia ya Masafa (Miaka 03 hadi 04).

Mafunzo haya yatatolewa katika **Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali**. Wizara inakaribisha maombi ya kujiunga na Mafunzo ya Ualimu katika Vyuo vya serikali na visivyo vya serikali kwa kuzingatia sifa zilizobainishwa katika tangazo hili.

## 2. SIFA ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU

a) Sifa za kujiunga na Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Msingi (Miaka 02) ni:

(i) Wahitimu wa Kidato cha sita wenye ufaulu wa Daraja la I-III kwa kiwango cha **“Principal Pass”** mbili (02); na

(ii) Walimu waliohitimu Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Astashahada (Cheti) ya Ualimu Elimu ya Awali au Msingi. Aidha waombaji wa mafunzo watakaochaguliwa, watapangwa kwenye mikondo kulingana na ufaulu wao katika Mtihani wa Taifa wa Ualimu ngazi ya Astashahada ya Elimu ya Ualimu.

b) Sifa za kujiunga na Stashahada Maalumu ya Ualimu Elimu ya Msingi (Miaka 03) ni wahitimu wa Kidato cha nne wenye ufaulu wa Daraja la I-III kwa kiwango cha alama “C” au zaidi katika masomo matatu, mawili kati yake yakiwa ni: ***Basic Mathematics, Biology, Chemistry, Physics, Information and Computer Studies au Computer Science***.

c) Sifa za kujiunga na Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Msingi kwa njia ya Masafa (Miaka mitatu (03) hadi minne (04) ni walimu waliohitimu Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Astashahada (Cheti) ya Ualimu Elimu ya Awali au Msingi.

Vyuo vya Ualimu vyenye nia ya kuendesha Mafunzo ya Ualimu kwa njia ya masafa vitapaswa kuzingatia masharti ya *Mwongozo wa Utoaji wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Awali na Msingi kwa njia ya Masafa (Feb.2026)* uliotolewa na Kamishna wa Elimu.

## 3. AINA YA MAFUNZO NA VYUO VINAVYOTOA MAFUNZO

Jedwali lifuatalo linaonesha aina ya Mafunzo ya Ualimu (kozi) na vyuo vinavyotoa mafunzo husika.

## A. STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI NA MSINGI (MIAKA 02)

| Na. | AINA YA MAFUNZO (KOZI) | VYUO VINAVYOTOA MAFUNZO | |
|---|---|---|---|
| | | Vya Serikali | Visivyo vya Serikali |
| 1 | Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa Sayansi ya Jamii (kwa kutumia lugha ya kiswahili) | Mhonda Bustani Murutunguru Mpuguso na Vikindu | Al harmain, Darmiki, Nyamwezi, Montessori Kawekamo, St. Aggrey Chanji, Mong'are, Lake, Bishorp Daniel, King Rumanyika, Kilimanjaro modern, Tusaale, Singida, Kirinjiko na King'ori |
| 2 | Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa Sayansi ya Jamii (kwa kutumia lugha ya Kiingereza) | Mpuguso na Shinyanga | UCA na Lake |
| 3 | Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa Sayansi ya jamii na lugha ya kiswahili (kwa kutumia lugha ya kiswahili). | Bunda na Tandala | St. Aggrey, St. Marys, Coast, Green bird, Nazareth, TEKU, St. Maurus, Arafah, Sila, Lua Kisongo, Mwl. Franz, St. Francis Nkindo, Sahara, Lake Mbeya Moravian, Rukwa, DC Brilliant, Ebonite, Arusha, Mtumba, Singida na Musoma Utalii |
| 4 | Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa Sayansi na Hisabati (kwa kutumia lugha ya kiingereza) | Tabora na Mandaka | UCA |
| 5 | Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa Sayansi na Hisabati (kwa kutumia lugha ya kiswahili) | Kitangali na Ndala Mamire na Sumbawanga | St. Aggrey, Sila, St. Marys, Coast, Green bird, Teofilo Kisanji, St. Maurus, Arafah, Kisongo, Mwl. Franz, St. Francis Nkindo, Nyamwezi, Sahara, Mbeya Moravian, Rukwa, Ebonite, Arusha, DC Brilliant, Mtumba, Montessori Kawekamo, Musoma Utalii, Al harmain, St. Aggrey Chanji, Lake, Bishorp Daniel, King'ori, Kirinjiko, King Rumanyika, Kilimanjaro modern na Singida, Partage Montessori. |
| 6 | Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali (kwa kutumia lugha ya kiingereza) | Dakawa na Nachingwea | UCA na Partage Montessori. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7 | Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali (kwa kutumia lugha ya kiswahili) | Kinampanda Katoke Singachini | Darmiki, Partage Montessori, Tusaale, King Rumanyika, Singida na Kilimanjaro modern |
| 8 | Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa lugha (Kiingereza, Kifaransa na Kichina) | Marangu | Arafah, St. Aggrey Chanji, UCA, King'ori, Bishorp Durning, King Rumanyika, Nyamwezi, Al Harmain, Kilimanjaro modern na Montessori Kawekamo |
| 9 | Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa Sanaa na Michezo (kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili) | Butimba | |
| 10 | Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa Sanaa na Michezo (kwa lugha ya kiswahili) | Ilonga na Tarime | Lake, Montessori Kawekamo, King Rumanyika, Coast, Nyamwezi na Musoma Utalii |
| 11 | Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu (kwa kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza) | Patandi | |
| 12 | Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu (kwa kutumia lugha ya kiswahili) | Kabanga na Mpwapwa | |

**B. STASHAHADA MAALUMU YA UALIMU ELIMU YA MSINGI KATIKA MASOMO YA SAYANSI NA HISABATI (MIAKA 03)**

| Na | AINA YA MCHEPUO | VYUO VINAVYOTOA MAFUNZO |
|---|---|---|
| 1. | PME, CBE, CME na CSME | Tukuyu na Butimba |
| 2. | PME, PCE, PBE, CBE, CME na CSME | Morogoro, Kasulu, Songea, Korogwe na Tabora |
| 3. | PME, PCE, PBE, CME na CBE | Klerruu na Monduli |

## 4. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI NA KUPOKEA MAJIBU

Utaratibu wa kutuma maombi na kupokea majibu kwa waombaji wa Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Msingi na Stashahada Maalumu ya Elimu ya Msingi utakuwa kama ifuatavyo:

(i) Wahitimu wa Kidato cha nne, Kidato cha sita na Walimu waliohitimu Astashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Msingi, wenye sifa zilizobainishwa katika tangazo hili wanaruhusiwa kutuma maombi;

(ii) Waombaji wa Mafunzo ya Ualimu katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali wanatakiwa kujisajili na kutuma maombi kielektroniki kupitia mfumo wa udahili wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (**https://tcm.moe.go.tz/**);

(iii) Mwombaji wa Mafunzo ya Ualimu ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Msingi (Miaka 02) atachagua michepuo mitatu (03) kwa kuanza na ule anaoupenda zaidi;

(iv) Mwombaji wa Mafunzo ya Ualimu ya Stashahada Maalumu ya Ualimu Elimu ya Msingi (Miaka 03) atachagua tahasusi tatu (03) kwa kuanza na anayoipenda zaidi;

(v) Majibu kwa watakaochaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Ualimu katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali yatatolewa kwenye mfumo kupitia "**Account**" aliyotumia mwombaji kuomba mafunzo ya Ualimu (kuanzia tarehe **15/07/2026**) na katika Vyuo vya Ualimu walivyochaguliwa;

(vi) Waombaji wa Mafunzo ya Ualimu katika Vyuo visivyo vya serikali watatuma maombi katika vyuo husika. Aidha, majibu kwa watakaochaguliwa kujiunga na Mafunzo hayo yatatolewa na Vyuo vya Ualimu walivyochaguliwa; na

(vii) Fomu za maelekezo ya kujiunga na Mafunzo ya Ualimu zitatolewa kupitia tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (www.moe.go.tz) na Chuo atakachopangwa mwombaji kwa kutumia anuani yake. Waombaji wote wanashauriwa kuandika anuani kamili, barua pepe na namba ya simu inayopatikana kwa mawasiliano.

(viii) Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **10/07/2026.**

Digitally Signed By Prof.Carolyne I. Nombo
Tue Jun 09 18:14:26 EAT 2026

Prof.Carolyne I. Nombo
**KATIBU MKUU**